JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

04 HISABATI

Muda: Saa 1: 30 **Mwaka: 2018.**

Maelekezo

1. Mtihani huu una jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**
3. Kila swali lina **alama (10)**

Na.		Swali	Nafasi ya Kazi	Jibu
1.	(a)	Andika namba 20,392 kwa maneno.		
	(b)	Andika XXXIV kwa namba za Kiarabu.		
	(c)	Andika thamani ya tarakimu iliyopigiwa mstari katika namba 3<u>4</u>02.		
	(d)	Andika namba ifuatayo kwa kirefu: 9536		
	(e)	Wanafunzi walipanda miti 680 ili kulinda mazingira ya shule.Andika idadi ya miti iliyopandwa kwa maneno.		
2.	(a)	Jaza namba inayofuata katika mpangilio wa namba zifuatazo:1, 3, 5, 7, _____.		
	(b)	Panga namba zifuatazo kwa mpangilio unaoanza na namba ndogo hadi namba kubwa zaidi: 20, 4, 12, 7, 16, 3, 10.		
	(c)	Andika namba inayokosekana ili kukamilisha mpangilio wa namba za Kirumi ufuatao: XXII, XXV, XXVIII, _, XXXIV.		
	(d)	Andika namba inayokosekana katika mfululizo ufuatao: 36, 33, 30, ___, 24.		

Na.		Swali	Nafasi ya Kazi	Jibu
	(e)	Chura aliruka hatua tatu zenye urefu sawa hadi kufikia m 21. Ikiwa aliruka hatua ya nne yenye urefu sawa na hatua za mwanzo, je, alifikia umbali gani?		
3.	(a)	Jumlisha; 1715 + 263 =		
	(b)	Gawanya; 20) 600		
	(c)	Shule ya msingi Mkombozi ina wanafunzi 826. Ikiwa idadi ya wavulana ni 408, je, wasichana ni wangapi?.		
	(d)	Zidisha; 49 x 53 =		
	(e)	Kijo alikuwa na shilingi 9,750. Alimpa rafiki yake kiasi Fulani cha fedha na kubakiwa na shilingi 3,250. Je, alimpa rafiki yake shilingi ngapi?		
4.	(a)	Andika jina la umbo lifuatalo ambalo urefu wa pande zake zote nne zinalingana: 		
	(b)	Sehemu zilizogawanywa katika umbo lifuatalo zinalingana. Andika sehemu iliyowekwa kivuli. 		

Na.		Swali	Nafasi ya Kazi	Jibu
	(c)	Tafuta mzingo wa umbo lifuatalo:  		
	(d)	Mzingo wa pembetatu ni sm 48. Ikiwa urefu wa upande wa kwanza ni sm 12 na urefu wa upande wa pili ni sm 20, tafuta urefu wa upande wa tatu.		
	(e)	Mstatili una mzingo wa sm 80 na urefu wa sm 25. Tafuta upana wake.		
5.	(a)	Jumlisha; Sh. 1940 + sh. 265=		
	(b)	Toa; Sh. 3150 - sh. 1500=		
	(c)	Zidisha; Sh 3 0 0 × 2 5		
	(d)	Mariamu alikuwa na shilingi 8,650. Baadaye, alitumia shilingi 3,800. Je, alibakiwa na shilingi ngapi?		
	(e)	Noti ya Tanzania ya shilingi 10,000 ina noti ngapi zenye thamani ya shilingi 1,000?		